



DAR ES SALAAM STOCK EXCHANGE PLC

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA NNE WA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Nne wa Wanahisa wa Kampuni ya Soko la Hisa la Dar Es Salaam utakaofanyika Hoteli ya New Africa iliyopo kona ya Mtaa wa Azikiwe na barabara ya Sokoine Dar Es Salaam, siku ya Jumatano tarehe 25 Juni 2019 kuanzia sa tatu na nusu asubuhi (9.30 a.m.) kwa madhumuni yafuatayo:

1. Kupisha ajenda ya mkutano;
2. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Tatu wa Mwaka;
3. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Tatu wa Mwaka;
4. Kupokea na kupitisha
 - 4.1 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya DSE kwa Mwaka uliyoishia tarehe 31 Disemba, 2018;
 - 4.2 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya DSE na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2018;
 - 4.3 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya *Fidelity Fund* na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2018;
5. Kupitisha Malipo ya Wakaguzi wa Nje;
6. Uteuzi wa Wakaguzi wa Nje kwa Mwaka wa Fedha 2019;
7. Kuidhinisha Malipo ya Ada ya Wakurugenzi kwa Mwaka wa Fedha 2019;
8. Kuidhinisha Malipo ya Gawio kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2018;
9. Kuchagua Wajumbe Wapya wa Bodi ya Wakurugenzi ya DSE; na
10. Mengineyo.

Maelezo

1. Mwanahisa atakaye hudhuria mkutano atatakiwa kufika na nakala ya *Depository Receipt* pamoja na kitambulisho chake.
2. Vitabu vyenye taarifa za hesabu kwa mwaka 2018 pamoja na fomu ya mwakilishi vitapatikana katika Ofisi za DSE, Ghorofa ya 3, Jengo la Kamarage, Mtaa wa Ufukoni na kwa Madalali wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam kuanzia Jumatatu tarehe 10 Juni 2019.
3. Mwanahisa yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano ana haki ya kuchagua mwakilishi au wawakilishi na kupiga kura kwa niaba yake. Endapo mwanahisa ni shirika, mwakilishi anatakiwa kuwa na fomu za uwakilishi ziwe zimegongwa muhuri wa kampuni. Fomu hizo zifikishwe kwa Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi katika ofisi za DSE kabla ya saa nane mchana (02:00 p.m.) Jumatatu tarehe 24 Juni 2019.
4. Orodha (Register) ya Wanahisa watakaostahili kupiga kura itafungwa Jumatatu tarehe 19 Juni 2019.

Kwa Agizo la Bodi

Mary Stephen Mniwasa
Katibu wa Bodi
4 Juni 2019